MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA WAZABUNI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 03 mwezi 02 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha VETA - MARA, S.L.P. 188, MUSOMA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 DODOMA (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

MWITA KIBACHO MGAMBI S.L.P. 186, BUNDA (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni") kwa upande mwingine

**KWA KUWA** Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA;

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA;

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya majadiliano na kukubaliana na Mzabuni kwa ajili ya kuleta vifaa ya ujenzi VIGAE;

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

1. **GHARAMA YA VIFAA**
   Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 59,810,800'00, Mzabuni atawakilisha vifaa vifuatavyo kwenye eneo la ujenzi.

| | | |
|---|---|---|
| Skirting (600 mm long; 25No/Box)(Black in color) Twyford Grade one | Box | 210 |
| 500 x 500 x 8mm Porcelain floor tiles Twyford Grade one | Box | 1020 |
| 200mmx300mmx6mm thick ceramic Wall tiles-Twyford grade one | Box | 352 |
| Tile grout | PCKT | 120 |
| Strips | Pc | 60 |

## 2. MABADILIKO YA GHARAMA ZA MANUNUZI YA VIFAA VYA UJENZI

Gharama ya vifaa vya ujenzi haitabadilika ndani ya kipindi cha muda wa MIEZI mitatu tokea tarehe ya kufunga mkataba huu.

## 3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

i. Mwajiri atamlipa Mzabuni kwa kutumia Mfumo wa Ulipaji Serikalini(MUSE) kabla ya kupeleka vifaa kwenye eneo la ujenzi.

ii. Mwajiri atalazimika kukata kodi ya zuio **asilimia mbili** (2%) "Withholding Tax" ambayo ni makato yaliyopo kisheria

## 4. MAKABIDHIANO YA VIFAA VYA UJENZI

(a) Vifaa vitakabidhiwa kwenye eneo la ujenzi ndani ya siku....21.......mara tu baada ya malipo kulipwa kwa Mzabuni pindi Mzabuni atapokuwa anawasilisha vifaa kwenye eneo la ujenzi, pande zote mbili zitaweka kumbukumbu za maandishi wakati wa makabidhiano na kusaini katika daftari maalum.

(b) Pindi vifaa vitapofika kwenye eneo la ujenzi vitakaguliwa na Kamati ya Mapokezi ili kujiridhisha vitu vifuatavyo.

i. Ubora wa vifaa
ii. Idadi ya vifaa
iii. Muda wa Ukomo wa matumzi wa vifaa
iv. Kama kuna uharibifu wowote

## 5. WAJIBU WA MZABUNI

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kuwasilisha vifaa kwenye eneo la ujenzi ndani ya muda uliowekwa ambao ni siku ___21___

(b) Kubadilisha kifaa ambacho kitakuwa kimekutwa na mapungufu na kamati ya Mapokezi na kuleta kifaa kingine ambacho kitakuwa na sifa stahiki ndani ya

siku.....05.....

(c) Kwa Mzabuni anayelipwa baada ya kuwasilisha vifaa na kupokelewa na kamati ya Mapokezi ana stahili kulipwa malipo yake ndani ya siku 14.

(d) Kumjulisha Mwajiri kuhusu ucheleweshaji wa kuleta vifaa ndani ya muda.

6. **WAJIBU WA MWAJIRI**

Mwajiri atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kumlipa mzabuni malipo halali ya kazi iliyoainishwa katika Mkataba huu kulingana na utaratibu uliobainishwa katika kipengele Na.3 cha Mkataba huu.
(b) Kupokea vifaa ambavyo vimekidhi vigezo vyote kwa ajili ya ujenzi.

(e) Kuhifadhi na kutekeleza masharti yote ya Sheria za nchi zinazohusiana na kazi anayoifanya Mzabuni;

(c) Kumkata Mzabuni kodi ya zuio (withholding tax).

7. **MAMBO YALIYO NJE YA UWEZO WA KIBINADAMU**

Itakapotokea jambo lolote lililo nje ya uwezo wa kibinadamu kama vile mafuriko, kimbunga, tetemeko la ardhi na mambo yanayofanana na hayo, pande zote mbili zitapata nafasi ya kulijadili na kulipatia ufumbuzi wa haraka.

8. **SHERIA ZINAZOTUMIKA**

Sheria za kutafsiri Mkataba huu na ufanyaji wa kazi katika Mkataba huu ni Sheria za Tanzania.

9. **USIRI**

Nyaraka zote zitakazokuwa zimetumika katika ujenzi unaohusu Mkataba huu hazitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa ujenzi unaohusu Mkataba huu. Pia taarifa yoyote itakayopatikana wakati wa ujenzi unaohusu Mkataba huu haitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa ujenzi unaohusu Mkataba huu.

10. **USULUHISHI WA MIGOGORO**

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhisha mgogoro, basi upande wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi(arbitration).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MIHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA.....VETA MARA

Jina: DAVID LOUIS Saini: ____________

Wadhifa: MSIMAMIZI WA MRADI BUTIAMA DVTC Tarehe: 03 . 02 . 2022

MKUU WA CHUO VETA-MARA P.O.BOX 138 MUSOMA

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ALFRED G KIDIFU Saini: ____________

MKUU WA CHUO VETA-MARA P.O.BOX 138 MUSOMA

Wadhifa: AFISA MANUNUZI MSAIDIZI Tarehe: 03 . 02 . 2022

Jina: AZIZ. M. RUBARE Saini: ____________

Wadhifa: MIKITI KAMATI Tarehe: 03 - 02 - 2022.

IMESAINIWA NA MZABUNI

Jina: Kibacho Mugeni Saini: ____________

Wadhifa: Afisa Tilas hagati Tarehe: 3 . 2 / 2022

KIBACHO HARDWARE
P. O. Box 186 - BUNDA
TIN: 140-223-972

Mbele ya (Shahidi)

Jina: Musa Kebacho Saini: ____________

Wadhifa: Shahidi Tarehe: 3/2/2022